# BRELA

## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

JARIDA | ISSN: 00000401 | Toleo Na. 02 | Oktoba, 2021 - Machi, 2022



# MWAKA 1 MADARAKANI

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Usajili wa Kampuni za kitanzania | 11,348 |
| 2 | Usajili wa Kampuni za kigeni | 74 |
| 3 | Usajili wa Majina ya Biashara | 22,251 |
| 4 | Usajili wa Alama za Biashara na Huduma | 3,056 |
| 5 | Utoaji wa Leseni za Biashara kundi A | 12,704 |


# YALIYOMO


4 WAHIMIZWA KURASIMISHA BIASHARA





6 WATAKIWA KUTOA ELIMU KWA WAFANYABIASHARA



18 MAFANIKIO YA BRELA NA MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA





BODI YA UHARIRI

**Andrew Mkapa**
Mwenyekiti

**Roida Andusamile**
Katibu

**wajumbe**
Tawi Kilumile
Theresa Chilambo
Abdulrahman Songoro
Neema Kitala
Nehemia Mihayo

**Alpha Nuhu**
Mhariri Mstaafu - TSN


BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

# BRELA yaagizwa kuandaa mkakati wa soko la bidhaa



Mhe. Prof. Godius Kahyarara

**Na Roida Andusamile**

Serikali imeiagiza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kuandaa mkakati utakaowezesha soko la bidhaa kuwa na bei halali.

Mkakati huo, kupitia utoaji wa leseni za biashara, utaiwezesha BRELA kudhibiti na kujiridhisha na mnyororo wa usambazaji wa bidhaa, ufuatiliaji wa wafanyabiashara waliopo kwenye masoko na kuwaweka kwenye mfumo rasmi.

**"Tunapaswa kutumia kila silaha ili watanzania wasiumizwe kwenye bei, hivyo BRELA muanze kufikiri njia gani itumike ili hatimaye wauzaji wazingatie bei halali ya soko"**

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda Mhe. Prof. Godius Kahyarara, wakati akizungumza na menejimenti ya BRELA alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi za taasisi hiyo hivi karibuni Jjini Dar es Salaam.

Alisema taasisi za wizara hiyo zinapaswa kuwa na udhibiti wa masoko wenye lengo la kuleta usawa kuanzia kwa mzalishaji, msambazaji hadi kwa mlaji.

"Kama Serikali tunapaswa kuhakikisha kuwa kunakuwa na biashara ya haki kwa anayezalisha, anayeuza na mlaji na kama Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda bado suala la bei za bidhaa sokoni, halijafanyiwa kazi kikamilifu," alifafanua Prof. Kahyarara.

Aliongeza kuwa umefika wakati kwa taasisi kubadili taratibu za utendaji kazi, kwa sababu majukumu na matarajio yaliyopo ni makubwa, "na kwa hiyo tunatakiwa kuondokana na uchumi wa kivuli na kwenda kwenye uchumi wa nuru (from shadow to light economy).

Prof. Kahyarara alisisitiza kuwa licha ya kuwa na wafanyabiashara wengi, bado Serikali haijaweza kuwadhibiti kikamilifu kwa kuhakikisha kuwa wanafanyabiashara bila ya kuvunja sheria na taratibu zilizopo.

Aliongeza kuwa bila ya kuwa na udhibiti kwenye masoko wananchi wa kipato cha chini wataendelea kuumia na kwamba utafiti mdogo uliofanywa na wizara umebaini kuwa asilimia kubwa ya wanaopandisha bei za bidhaa ni wale wanaopeleka sokoni.

"Tunapaswa kutumia kila silaha ili watanzania wasiumizwe kwenye bei, hivyo BRELA muanze kufikiri njia gani itumike ili hatimaye wauzaji wazingatie bei halali ya soko," alisisitiza Prof. Kahyarara.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alimhakikishia Prof. Kahyarara kuwa BRELA itatekeleza agizo hilo kwa ukamilifu kwa kuzingatia majukumu pamoja na malengo ya taasisi kwa kuweka mifumo rasmi ambayo hatimaye itawasaidia wananchi



*Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara akizungumza na Menejimenti ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi hizo. Katika ziara hiyo Prof, Kahyarara alipokelewa na mwenyeji wake Bw. Godfrey Nyaisa, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA*

# Wahimizwa kurasimisha biashara



Na Christine Njovu

Wanawake wajasiriamali wametakiwa kurasimisha biashara zao ili waweze kutambulika na kupata fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali pamoja na taasisi zake, zikiwemo taasisi za kifedha.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa, alitoa wito huo hivi karibuni jijini Dar es Salaam wakati akifungua Kongamano la Wajasiriamali Wanawake lililofanyika kwa lengo la kuenzi Siku ya Mwanamke Mjasiriamali Duniani.

**"Urasimishaji biashara pia unasaidia kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii"**

"Naomba nitumie fursa hii kuwashauri na kuwasisitiza kuwa ni muhimu kurasimisha biashara zenu kwa kuwa kuna manufaa makubwa utayapata kutokana na urasimishaji kuliko kufanya biashara katika hali zisizo rasmi," alisisitiza Bw. Nyaisa.

Bw. Nyaisa aliainisha baadhi ya faida za urasimishaji biashara kuwa ni pamoja na biashara kutambuliwa na serikali, wateja na jamii kwa ujumla, kuongeza fursa za kupata huduma za serikali, kurahisisha upatikanaji wa mitaji kutoka serikalini na taasisi za fedha kama vile benki na taasisi zinazotoa mikopo.

Alizitaja faida nyingine kuwa ni kupata huduma mbalimbali za serikali kama vile, mafunzo, msaada wa kitaalamu na kiteknolojia.

Aliongeza kuwa endapo biashara itarasimishwa inaiwezesha serikali kuboresha mipango yake ya kuwahudumia wajasiriamali na wafanyabiashara kwa kuwa inakuwa na uelewa wa idadi kamili ya wajasiriamali au wafanyabiashara waliopo.

"Urasimishaji biashara pia unasaidia kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa serikali katika kutoa huduma kwa jamii," alifafanua Bw. Nyaisa

Aliongeza kuwa biashara inaporasimishwa inaongeza uaminifu kwa wateja kutokana na kutambulika na Serikali hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kuingia mikataba ya kibiashara ama ubia na wafanyabiashara wengine pamoja na Makampuni ya ndani na nje ya nchi sambamba na kurahisisha upatikanaji wa dhamana kutoka serikalini au taasisi binafsi.

Aidha Bw. Nyaisa alisema kuwa Serikali inatambua umuhimu wa wajasiriamali katika ujenzi



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa akifungua Kongamano la Ujasiriamali kwa ajili ya kuenzi siku ya Mwanamke Mjasiriamali Duniani lililofanyika katika ukumbi wa Golden Memory Jijini Dar es Salaam.*



*Baadhi ya Wanawake wajasiliamali wakimsikiliza Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa akifungua Kongamano la Ujasiliamali kwa ajili ya kuenzi siku ya Mwanamke Mjasiriamali Duniani lililofanyika katika ukumbi wa Golden Memory Jijini Dar es Salaam.*

wa uchumi endelevu, ukuaji wa biashara na kuongeza ajira kwa jamii ya Watanzania.

Kutokana na umuhimu wa wajasiriamali, Bw. Nyaisa alisema kuwa serikali inaendelea kufanya maboresho mbalimbali ya kisera, kisheria, kanuni, taratibu na mifumo ya utoaji huduma kwa kuzifanya kuwa wezeshi na rafiki kwa wafanyabiasha wakubwa na wadogo ili waweze kurasimisha biashara zao na kunufaika na fursa mbalimbali zinazotokana na urasimishaji huo.

"Wanawake wengi wamekuwa wakifanya biashara nyingi ndogondogo na nzuri na wamekuwa wakibuni nembo za biashara zao na kuzitumia kwa muda mrefu lakini ajabu ni kwamba hawazisajili , hali hii imepelekea baadhi ya watu kunakili majina ya biashara hizo na nembo na kuja BRELA kuchungulia kama zimesajiliwa na iwapo hazijasajiliwa basi wanasajili na kuzitumia , hali hii imesababisha wahusika kufikisha malalamiko BRELA," amefafanua Bw.Nyaisa.

Bw. Nyaisa aliongeza kuwa urasimishaji wa biashara unafanyika kwa kufanya sajili mbalimbali za kibiashara ikiwa ni pamoja na

Majina ya Biashara, Kampuni, Alama za Biashara na Huduma, utoaji wa Hataza, leseni za biashara na viwanda pamoja na usajili wa viwanda vidogo.

"Urasimishwaji huu unafanyika kwa njia ya mtandao ambapo kwa sasa mfanya biashara hahitaji kusafiri umbali mrefu kupata huduma, maboresho haya tuyatumie kama fursa kwa kuwa sasa sajili zote na utoaji Leseni unafanyika ndani ya muda mfupi sana," amefafanua Bw. Nyaisa.

Kongamano hilo lililoratibiwa na taasisi ya Youth Dreams

Foundations limewakutanisha Wajasiriamali Wanawake wa Jiji la Dar es Salaam, ambao wamenufaika na mada mbalimbali zilizotolewa kuhusiana na ujasiriamali.






*Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Mhandisi Robert Gabriel akifafanua jambo wakati akifungua mafunzo ya Maafisa Biashara wa mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara na Simiyu.*

# Watakiwa kutoa elimu kwa wafanyabiashara

**Na Christina Njovu**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhandisi Robert Gabriel amewataka Maafisa Biashara nchini kutoa elimu kwa wafanyabiashara kwa kufungua dirisha la Biashara ili kukuza sekta hiyo na kufufua matumaini yao.

Mhandisi Gabriel alitoa wito huo wakati wa kufungua mafunzo ya Sheria za Leseni za Biashara kwa Maafisa Biashara wa mikoa ya Kanda ya Ziwa ikiwemo mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara na Simiyu yaliyoendeshwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) mkoani Mwanza.

Alisisitiza umuhimu wa Maafisa Biashara kutoa elimu kwa wananchi ambayo ni nyenzo muhimu ya kupunguza kero mbalimbali na gharama za urasimishaji biashara, suala ambalo Serikali imekuwa ikilipigia kelele kwa nguvu zote.

**"Mafunzo haya yatoe matunda na kuonesha muelekezo mzima wa utatuzi wa changamoto na lenye kuleta ongezeko la wafanyabiashara na kukuza biashara nchini kimpango kazi na kuonesha muelekeo mzima wa utatuzi wa changamoto na ongezeko la wafanya biashara na kukuza biashara nchini"**

"Ndugu zangu Maafisa Biashara kuna mtu amepata mtaji anataka aanze biashara mapema lakini unamuambia njoo kesho mara kesho kutwa anachanganyikiwa, tukumbuke kuwa mteja ni mfalme," alifafanua Mhe. Gabriel.

Aidha aliongeza kuwa ikiwa mfanyabiashara huyo ataambiwa njoo kesho mara kesho kutwa, utakuta fedha aliyonayo inapata matumizi mengine na kuiingiza katika kutatua changamoto aliyonayo kiasi kwamba anakwama katika kutimiza malego yake, Afisa biashara unapoonekana mahali uonekane kuwa ni msaada kwa wafanyabiashara, hivyo watatulieni changamoto zao.

"Fungueni dirisha maalum la kutatua changamoto za wafanya biashara na mnatakiwa kujipima kwa kila robo ya mwaka, msifanye kazi kwa mazoea (business as usual), kuweni na takwimu kuwa nina wafanya biashara wadogo wangapi, wakubwa wangapi na wale walio ICU (chumba cha mahututi) ni wangapi na kutafuta njia ya



*Mwanasheria kutoka Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Daniel Mwamlima, akitoa ufafanuzi kuhusu Sheria za Leseni katika mafunzo ya Maafisa Biashara wa Kanda ya Ziwa kutoka mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Simiyu.*

kuwasaidia ili waweze kurudi katika hali zao za kibiashara," amesisitiza Mhandisi Gabriel.

Aliongeza kuwa kwa utafiti mdogo uliofanyika kuhusu utendaji kazi wa Maafisa Biashara umebaini kuwa kumekuwa na uelewa hafifu wa Sheria ya Leseni za Biashara sura ya 208, na Maafisa Biashara wengi kutumika kama wakusanyaji mapato hasa vilabuni, maduka makubwa na nyumba za kulala wageni, kiasi cha kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kazi wazifanyazo haziusiani na majukumu yao.

Mhe. Gabriel alisema ni vema Maafisa Biashara wakafuatilia mafunzo hayo ambayo hayajaandaliwa kwa bahati mbaya bali ni mkakati maalumu wa kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa na Maafisa Biashara zinatoa nafasi kwa wafanyabiashara kuimarika kibiashara na kupata fursa ya kushiriki katika kuchangia pato la taifa ambalo litatumika kutoa huduma kwa wananchi katika mkakati mahususi wa blue print.

Aliwataka Maafisa biashara kuleta faida ya mafunzo haya kwa kuandaa mpango kazi maalumu, Mafunzo haya ya siku tano yatoe matunda, mafunzo haya yakawe kimpango kazi na kuonesha muelekeo mzima wa utatuzi wa changamoto na ongezeko la wafanya biashara na kukuza biashara nchini.

**"Ndugu zangu Maafisa Biashara kuna mtu amepata mtaji anataka aanze biashara mapema lakini unamuambia njoo kesho mara kesho kutwa anachanganyikiwa, tukumbuke kuwa mteja ni mfalme"**

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa akimkaribisha Mhandisi Gabriel kufungua mafunzo hayo alisema lengo ni kuwajengea uwezo maafisa biashara wa Mikoa na Halmashauri zote nchini ili waweze kuielewa vema Sheria ya Leseni za Biashara sura namba 208 na kuweza kutoa huduma bora kwa wafanyabiashara na kusaidia kutoa huduma za Serikali kwa wananchi ili kuboresha mazingira ya biashara.

Bw. Nyaisa aliongeza kuwa BRELA inaendelea na uboreshaji wa utoaji wa huduma zake na kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini, kwa sasa huduma zote za BRELA zinapatikana kwa njia ya mtandao kupitia mifumo miwili unaojulikana kama Online Registraton System (ORS) kwa Sajili na Leseni za Viwanda na Tanzania National Business Portal (TNBP) kwa utoaji wa Leseni za Biashara.

Aidha mfumo wa utoaji wa Leseni za Biashara (National Business Portal-NBP) unafanyiwa maboresho ili uweze kutumika kutoa huduma za Leseni za Biashara katika Halmashauri zote nchini kwa utoaji wa Leseni za Biashara za kundi "B" ambapo hatua hii itaboresha mazingira ya biashara nchini na kuwapunguzia gharama wajasiriamali na wafanyabiashara.

Aidha aliwataka Maafisa Biashara kubadilika kama ambavyo wito umekuwa ukitolewa na Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuwasisitiza watumishi wa umma kubadilika na kuwa mfano bora kwenye utendaji kazi na uwajibikaji.

TAARIFA KWA UMMA

# Uwasilishaji wa taarifa za mwaka za kampuni

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa mujibu wa kifungu cha 128 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212 kila kampuni iliyosajiliwa hapa nchini (Locally Registered Company) inapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Kampuni Taarifa za Mwaka (Annual Returns) kila ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa (anniversary of incorporation) au tarehe nyingine ambayo Kampuni itakuwa imechagua na imemtaarifu Msajili na kukubaliwa.

Pia, Kampuni zilizosajiliwa nje ya nchi (Companies incorporated outside Tanzania) na kufungua ofisi hapa nchini, zinatakiwa kuwasilisha Mahesabu ya Mwaka (Annual Accounts) kwa mujibu wa kifungu cha 438 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Taarifa ya Mwaka husaidia kutoa taswira halisi ya kampuni na hivyo kusaidia umma kupata taarifa sahihi za kampuni kama vile taarifa za Wakurugenzi, Ofisi za Kampuni na wamiliki wa kampuni.

Kwa muongozo huu wa Sheria, endapo kampuni itashindwa kuwasilisha Taarifa ya Mwaka au Mahesabu ya Mwaka itatafsiriwa kuwa:

- Haifanyi biashara hapa nchini (dormant company) na hivyo kupelekea Msajili wa Kampuni kuiondoa kwenye Regista ya Kampuni hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 400 cha Sheria ya Makampuni, Sura 212; au
- Endapo Msajili atagundua kuwa kampuni ni hai na haijawasilisha Taarifa ya Mwaka kwa wakati zaidi ya siku ishirini na nane (28) ya tarehe ya kuwasilisha, kampuni itatakiwa kulipa faini kwa kila mwezi na sehemu ya mwezi itakayochelewa kuleta taarifa hiyo.
- BRELA inawahimiza Wakurugenzi na Makatibu wa Kampuni kuwasilisha taarifa ya Mwaka ya kampuni ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

# Wahimizwa kutumia kampuni zilizosajiliwa BRELA

**Na Roida Andusamile**

Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi hapa nchini wametakiwa kutumia kigezo cha kuhakiki uhalali wa kampuni zinazoomba zabuni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) wakati wa kufanya tathmini ya kampuni hizo.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa alitoa wito huo katika mkutano wa 12 wa Wataalam wa Ununuzi na Ugavi uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) Jijini Arusha.

Bw. Nyaisa alisema kumekuwa na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya kampuni zinazotaka kufanya kazi na Serikali hivyo ni muhimu kuthibitisha uhalali wake kabla ya kufanya maamuzi, hivyo ni vyema kuweka kigezo cha uthibitisho wa kampuni husika kutoka BRELA.

"Kuna baadhi ya kampuni hufunguliwa baada ya kusikia kuna kazi fulani inatafuta mzabuni hivyo kampuni za aina hiyo zinaweza kuwa na changamoto katika utendaji kazi kutokana na kutokuwa na uzoefu wa kazi husika, Wataalamu wa Ununuzi na ugavi hakikisheni kuwa kigezo cha taarifa za kampuni kutoka BRELA kinaambatishwa," alifafanua Bw. Nyaisa.

Bw. Nyaisa alisema mbali na kupata kazi mbalimbali Serikalini kampuni zinaposajiliwa na BRELA inakuwa rahisi kupata fursa za mikopo kutoka katika mabenki kwa sababu mabenki hufanya uchunguzi wa kampuni inayohitaji mkopo kwa kupata taarifa za kampuni husika kutoka BRELA.

Alisema mpaka sasa BRELA imekwishasajili kampuni 150,000 na mifumo ya usajili kwa njia ya mtandao inaendelea kuboreshwa ili kuondoa changamoto ndogondogo zinazojitokeza wakati wa usajili kwa njia ya mtandao.

**"Kuna baadhi ya kampuni hufunguliwa baada ya kusikia kuna kazi fulani inatafuta mzabuni hivyo kampuni za aina hiyo zinaweza kuwa na changamoto katika utendaji kazi kutokana na kutokuwa na uzoefu wa kazi husika, Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi hakikisheni kuwa kigezo cha taarifa za kampuni kutoka BRELA kinaambatishwa"**

# Watakiwa kubadilika kifikra na kiutendaji katika kutekeleza majukumu yao




*Mkurugenzi wa Leseni wa Wakala wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Andrew Mkapa, akifafanua jambo wakati akifunga mafunzo ya Maafisa Biashara wa mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara na Simiyu.*

**Na Christine Njovu**

**Mkurugenzi wa Leseni kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Andrew Mkapa, amewataka Maafisa Biashara kubadilika kifikra na kiutendaji na kuendeleza dhana ya kusaidia zaidi kuliko kufanya ubabe katika kutekeleza majukumu yao ya utoaji wa leseni za biashara.**

Bw. Mkapa ametoa wito wakati wa ufungaji wa mafunzo juu ya Sheria za Leseni za Biashara kwa Maafisa Biashara wa mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Mara na Simiyu yaliyoandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) mkoani Mwanza.

"Katika mapendekezo mengi mmetoa ushauri na maoni ambapo ukiangalia kwa asilimia kubwa yapo ambayo ni ya kisheria, yanayohitaji mchakato wa kisheria, yapo ya kisera yanayohitaji uboreshaji wa Sera lakini pia yapo yakiutendaji yanahitaji mabadiliko ya utendaji katika ofisi zetu, lakini yapo mengine ya kifikra tu ambayo yanahitaji kubadilisha fikra na mitazamo" alisema Bw. Mkapa na kuongeza kuwa

Kwa yale ambayo hayahitaji kusubiri michakato mingine mkajitahidi kwenda kubadilisha utendaji kifikra na mkaendeleze dhana ya kusaidiana zaidi badala ya kuonesha ubabe na mkajiandae kisaikolojia kwa ajili ya mabadiliko ya mifumo," alisema Bw. Mkapa.

Akitoa ufafanuzi wa sheria, Bw. Mkapa alieleza kuwa Sheria ya Leseni ya mwaka 1972 imekuwa ikifanyiwa mapitio mara kwa mara, lakini kwa asilimia kubwa mapitio yaliyokuwa yanafanyika chini ya sheria za fedha ya kila mwaka yanagusa masuala ya makusanyo ya mapato kwa asilimia kubwa, lakini mabadiliko hayakutokea huko tu bali yalitokea maeneo mengi kwenye maeneo ya kijamii na kiutendaji, hivyo kuna haja kubwa ya kufanyiwa mapitio na marekebisho ya sheria hii.

Aidha aliongeza kuwa kwa muda mrefu sheria hii unaweza sema ilikuwa haitumiki ama ilikuwa ikitumika kifungu kimoja na kutolea mfano wa mwaka 2004 Ada za Leseni ziliondolewa ambapo mtu alikuwa akikata Leseni mara moja tu na alikuwa haihuishi kwa maana ya kurenew na ilikaa hivyo hadi mwaka 2014, ndio maana sheria hii inaonekana ina mambo mengi ya kizamani na haipewi kipaumbele cha kufanyiwa maboresho kama zilivyo sheria nyingine.

Bw. Mkapa ameainisha kuwa moja ya sababu ambayo huenda imechangia kutofanyiwa marekebisho sheria ya Leseni ni wazo lililokuja la uanzishwaji wa sheria ya Bara (Business Activities Registration Act), ambayo kwa bahati mbaya haikuwahi kufanya kazi, lakini sheria hii katika vifungu vyake vya mwanzo ilionekana kuwa ilikuja kuchukua nafasi ya sheria hii ya Leseni za Biashara (Business Licence), hivyo kama ingepitishwa ingechukua nafasi na hii ndiyo sababu imefanya watu kutokuwa na msukumo wa kufanyia marekebisho kwa sheria iliyopo na kiuhalisia sheria hii inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Hata hivyo, Bw. Mkapa amebainisha kuwa kuna mchakato ambao umeanza kwa ajili ya kuifanyia marekebisho ili kuifanya iendane na wakati lakini pia kutoa toleo lililojumuisha marekebisho yote yaliyofanyika katika sheria hii

## TAARIFA KWA UMMA

# Kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika wa kampuni

**1. Kuhusu Mmiliki Mnufaika Katika Kampuni**

Kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, ili kampuni iweze kufanya biashara nchini inapaswa na Wakala wa Usajili wa Makampuni na Biashara (BRELA). Ili kupata usajili na mambo mengine,wahusika hupaswa kuwasilisha taarifa mbalimbali ikiwemo majina na wasifu wa wamiliki na wanahisa wa kampuni husika. Kwa mujibu wa Sheria hii, taarifa za kampuni huwekwa wazi katika daftari ya msajili na mtu yeyote anaruhusiwa kupekua daftari kama anahitaji kupata taarifa za kampuni husika.

Hata hivyo hapo awali wamiliki wa kampuni walikua hawalazimiki kuwasilisha taarifa za ziada za wanufaika wengine wa kampuni. Uzoefu unaonesha kuwa majina yanayowasilishwa katika usajili wa kampuni ni majina ya waendesha kampuni na wakati mwingine majina ya wamiliki halisi na wanufaika wakubwa wa kampuni hizo hayapo katika daftari la msajili. Mmiliki Mnufaika ni mtu ambaye si lazima aonekane kwenye nyaraka za makampuni lakini anamiliki, anafanya maamuzi, anahodhi au anaendesha asilimia kubwa ya uwekezaji kwenye kampuni au makubaliano ya kibiashara. Aidha, Benki ya Dunia na Taasisi nyingine za Kimataifa zinazohusika na masuala ya biashara zimesisitiza umuhimu wa kuongeza uwazi na uwajibikaji katika umiliki wa makampuni, ikiwemo kutambua wamiliki halisi wanufaika katika kampuni.

**2.Marekebisho ya Sheria ili Kupata Taarifa za Wamiliki Wanufaika**

Kama sehemu ya juhudi za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na katika kuendelea kukabiliana na uhalifu wa kiuchumi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Sheria ya Fedha, 2020 (Finance Act, 2020), lilipitisha marekebisho ya Sheria ya makampuni, Sura ya 212 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wamiliki Wanufaika (Beneficial Owners) katika kampuni zilizosajiliwa hapa nchini.

Katika kutekeleza marekebisho haya ya Sheria, Kifungu cha 459A Cha marekebisho hayo , zikitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni kuanza kuwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika (Beneficial Owners). Kanuni za kutekeleza Sheria hii zilikamilika mwaka jana mwezi Mei na makampuni yalipewa miezi sita yawe yamekamilisha taarifa hizo. Hata hivyo kutokana na upya wa dhana ya Mmiliki Mnufaika, Makampuni mengi hawakuweza kuwasilisha taarifa zao na yameleta maombi ya kuongezewa muda. Hadi tarehe 3 Januari, 2022 ni makampuni 14,026 pekee yameweza kuwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika kwa Msajili wa Makampuni, ambayo ni sawa na asilimia 14 ya matarajio

**3.Kuongeza Muda wa Kuwasilisha Taarifa za Wamiliki Wanufaika**

Kutokana na changamoto zlizojitokeza, na kwa kuzingatia maombi ya wafanyabiashara wengi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha taarifa husika, na kwa mamlaka niliyonayo kwa mujibu a kifungu cha 459A (2) Cha Sheria ya Makampuni, Sura ya 212, nimeamua kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika (Beneficial Owners) kwa muda wa miez sita (6) kuanzia tarehe 1 Januari, 2022.

Naielekeza BRELA itumie nafasi hii kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha umma na wamiliki wa kampuni kuhusu dhana, umuhimu na faida za kuwasilisha taarifa za Mmiliki Mnufaika. Aidha ninawahimiza wamiliki wa makampuni wote kutekeleza matakwa ya Sheria nilioyataja hapo juu ndani ya kipindi hiki cha nyongeza.

**Prof, Kitila Mkumbo (Mb),**
**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**
**4 Januari, 2022, DODOMA.**

BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

FAHAMU KUHUSU MFUMO WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WAMILIKI WANUFAIKA

Mfumo wa kupokea taarifa za Wamiliki Wanufaika ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa Online Registration System (ORS) hivyo kampuni ambazo zina maombi yanayoendelea kwenye ORS bado zinaweza kuwasilisha taarifa zake za Wamiliki Wanufaika kupitia link ya https://bo.brela.go.tz

"TUNAIPA UTU WA KISHERIA BIASHARA YAKO"

# BRELA yashiriki wiki ya ijue Tanzania Expo 2020 Dubai

**Na Theresa Chilambo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ni miongoni mwa taasisi za serikali zilizoshiriki katika Wiki ya Ijue Tanzania katika Maonesho ya Expo 2020 Dubai.

Ushiriki huo ulitokana na mwaliko kutoka kwa Mhe. Balozi Mohamed Mtonga, Balozi wa Tanzania nchini Abu Dhabi, UAE ambae alikuwa Kamishna Jenerali wa Banda la Tanzania kwenye Maonesho ya Expo 2020 Dubai ambapo alizialika Taasisi za Serikali kushiriki tukio hilo.

Lengo la mwaliko huo ni kuweza kuonesha juhudi zinazofanywa na Serikali ili kuweza kuvutia wawekezaji nchini na pia kuwaunganisha wafanyabiashara wa Tanzania na nchi zingine.

Wawakilishi walipokea taarifa iliyowasilishwa na Mkurugenzi wa Banda la Tanzania Bi. Getrude Ng'weshemi ambapo alieleza hali halisi ya ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo.

Taarifa iliweka bayana mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizopo na hatua zilizochukuliwa katika kuimarisha ushiriki wa dhati kwa Tanzania ili nchi iwe na manufaa kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Dubai (Diaspora) ambao walishiriki katika Siku maalum ya Uzinduzi wa Juma la "Ijue Tanzania'' katika kusherekea Siku ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Wakiwa kama wawakilishi wa kwanza wa Watanzania huko Dubai, walijitokeza na kuunga mkono jitihada za ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo ya Expo 2020 Dubai.

Pia wawakilishi wa taasisi walipita kwenye banda la Tanzania wakiongozwa na Mkurugenzi wa Banda hilo Bi. Getrude Ng'weshemi ambapo wajumbe waliweza kujionea maudhui ya vipaumbele vinavyoitangaza Tanzania katika Maonesho ya Expo 2020 Dubai.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wafanyabiashara na Wawekezaji kutoka Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji lililofanyika Dubai, UAE.*

Asilimia kubwa ya banda lilisheheni maudhui yanayoitangaza Tanzania kupitia Sekta za Utalii, Madini, Kilimo, Nishati, Utamaduni, Viwanda na Uwekezaji.

Vilevile, wajumbe wawakilishi wa Taasisi mbalimbali walipata wasaa wa kutembelea mabanda ya nchi za Thailand na Bostwana kwa lengo la kujifunza kutoka nchi hizo na kupata uzoefu wao wa kushiriki kwenye maonesho makubwa ulimwenguni kama hayo.

Hii ni fursa ya kipekee kwa nchi kujifunza, kupata uzoefu, kujitangaza na kukuza ushirikiano wa kidiplomasia na nchi nyingi za Bara la Afrika na dunia kwa ujumla.

Ushiriki huu unategemewa kuibua fursa mbalimbali ulimwenguni za kiuwekezaji na maendeleo endelevu kwa sababu katika kuunganisha fikra kuna uhakika wa kutatua changamoto na kukaribisha dunia yenye mafanikio.

Taasisi za sekta mbalimbali zilizoshiriki kwenye Maonesho ya Dunia ya Expo 2020 Dubai ni Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) pamoja na Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi, UAE.

# BRELA yafika Zanzibar

**Na Theresa Chilambo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imetoa rai kwa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kuitumia taasisi hiyo kurasimisha biashara zao.

Ushauri huo ulitolewa kwenye mkutano maalum wa kusikiliza changamoto kati ya taasisi wezeshi za biashara na wamiliki wa viwanda nchini katika Maonesho ya Sita ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania.

Afisa Mwandamizi kutoka Kurugenzi ya Miliki Bunifu ya BRELA Bw Raphael Mtalima alisema kwenye Maonesho hayo yaliyobeba kaulimbiu "Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania" kwamba taasisi yake inatoa huduma za Usajili wa Kampuni, Usajili wa Majina ya Biashara na Huduma, Kutoa Leseni ya Biashara Kundi A, Kutoa Leseni ya Kiwanda na Kutoa Hataza.

Wananchi wa Zanzibar waliipongeza BRELA kwa kushiriki katika maonesho hayo na kuwapa uelewa mpana hasa kwenye matumizi ya mfumo wa usajili kwa njia ya mtandano (ORS) na mfumo wa utoaji wa leseni za Biashara kupitia dirisha la Taifa la Biashara (TNBP)




*Wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria Zanzibar wakipata elimu ya namna BRELA inavyotekeleza majukumu yake walipotembelea banda la BRELA kwenye Maonesho ya Sita ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania yaliyofanyika Zanzibar katika Uwanja wa Maisara*

# Rasimisha biashara utambulike - Gondwe

**Na Sheila Mfunami**

Wafanyabiashara wamekuwa wakifanya biashara kwa kutumia majina ya biashara bila ya kuyarasimisha, hali inayosababisha wengi kutokutambulika kisheria na kusababisha kutoaminika kwenye taasisi za fedha pindi wanapohitaji huduma za mikopo.

Kauli hii ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe Godwin Gondwe (pichani), kwenye Maonesho ya One Stop Jawabu yaliyofanyika viwanja vya Posta, Kijitonyama jijini Dar es Salaam.

"Unapozungumzia majina ya biashara siyo lazima kwa mfanyabiashara kuwa na biashara kubwa sana; hata kama ndogo ila ni muhimu kusajili jina la biashara," alisema.



BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

Aliongeza kwa kuwa "unaposajili kampuni na alama za biashara kama mfanyabiashara unakuwa na alama ambayo inawakilisha biashara yako, hivyo inakuwa rahisi kwa mteja kuitambua."

Mhe, Gondwe alihitimisha kwa kuishukuru BRELA kwa kushiriki kwenye Maonesho hayo ili kuwafikia wafanyabiashara kwa karibu na kupata huduma zote zinazotolewa na BRELA kwa urahisi.

BRELA ilishiriki Maonesho hayo ambapo elimu na huduma za usajili wa makampuni, usajili wa majina ya biashara, usajili wa alama za biashara na huduma, utoaji wa leseni za biashara kundi A, utoaji wa leseni za viwanda, huduma za baada ya usajili na kupata leseni na huduma za kupata taarifa kwa mtandao zilitolewa.


BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI
UTARATIBU WA KUHUISHA TAARIFA ZA KAMPUNI
Ingia kwenye akaunti yako ORS kwa kutumia jina la mtumiaji na neno la siri, bofya Huduma mtandao chagua Kampuni, chagua kuwasilisha Mizania ya mwaka na hesabu kisha bonyeza endelea, ingiza namba ya kampuni kisha bofya tafuta.
JAZA TAARIFA ZA KAMPUNI KAMA IFUATAVYO
1. Jina la kampuni na anwani
2. Namba za vitambulisho vya taifa vya wakurugenzi na wanahisa
3. Namba za utambulisho wa mlipa kodi
4. Anwani ya makazi ya wakurugenzi na katibu wa kampuni
5. Namba za simu za wakurugenzi na wanahisa
6. Mtaji wa kampuni na mgawanyowa hisa kwa kila mwanahisa, kwa kampuni yenye mtaji
7. Katika sehemu ya viambatisho weka fomu namba 128, fomu ya majumuhisho au fom yamabadiliko ya taarifa za kampuni
BRELA tanzania  Brela _tanzania  brela _tanzania  ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz  www.brela.go.tz  +255-22 2212800  +255 (0) 735 331 003  BRELA ONLINETV


eMrejesho
Mfumo wa kutuma, kupokea na kufuatilia Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi.
#IAMBIE_SERIKALI
www.emrejesho.gov.go.tz
Pakua eMrejesho Mobile App
Ingia Katika Google Play
Tafuta emalalamiko
Tumia Msimbo
*152*00#
Chagua 9
Kisha 2
Serikali ya Kidigitali-Mahali Popote Muda Wote

# BRELA yawanoa wanafunzi wa MUM



*Afisa Usajili kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Yusuph Mwasakafyuka kitoa mafunzo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislam Morogoro (MUM) juu ya huduma zinazotolewa na taasisi hiyo na jinsi ya kuzipata kwa njia ya mtandao.*

**Na Nehemia Mihayo**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewapa mafunzo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM) jinsi ya kuingia katika ujasiriamali kabla au mara baada ya kumaliza masomo yao.

Akizungumza katika warsha hiyo, Afisa Usajili kutoka BRELA, Bw. Yusuph Mwasakafyuka alieleza kuwa urasimishaji wa biashara ni hatua ya kwanza na muhimu sana katika uanzishaji na uendelezaji wa biashara hatua ambayo ikirukwa inaweza kusababisha kuyumba au kuanguka kwa biashara badaye.

"Watu wengi wanafanya makosa wakati wa uanzishwaji wa biashara, mathalani kuanzisha na kutangaza biashara ambayo haijasajiliwa ni kinyume na taratibu kwa sababu kwa kufanya hivyo unaweza kuwa unavunja sheria kwa kutumia jina la mtu mwingine bila kujua au mtu mwingine anaweza kulisajili jina hilo na kulifanya lake kisheria" alisema Bw. Mwasakafyuka.

**"Elimu hii itawafungulia njia mpya wanafunzi wa chuo, badala ya kusoma masomo darasani pakee sasa wanapata fursa ya kufahamu pia upande wa pili wa kuna vitu gani wanapaswa kufanya, nawashukuru sana BRELA kwa elimu hii"**

Aidha Bw. Mwasakafyuka aliwatoa hofu kuhusu gharama za usajili wa kampuni na kueleza kuwa mtu anaweza kusajili kampuni akiwa na mtaji wa kuanzia shilingi za kitanzania elfu ishirini (20,000) na kuendelea na ada za usajili zimegawanyika katika makundi mbalimbali kulingana na mtaji husika.

"Ada za usajili wa kampuni sio kubwa kama watu wengi wanavyodhani na hii ni kwa sababu zimegawanywa kulingana na kiasi cha mtaji mfano kama mtu ana mtaji wa

kuanzia shilingi za kitanzania 20,000 hadi 1,000,000 atapaswa kulipa ada ya usajili ya 167,200" alifafanua Bw. Mwasakafyuka. Kwa upande mwingine pia kuna fursa ya kurasimisha biashara kwa wajasiriamali ambao hawajafikia hatua ya kufungua kampuni, hivyo wao wanaweza kusajili jina la biashara kama hatua ya kuanzia ambapo ada ya usajili ni shilingi ya kitanzania 20,000 pekee.

Kwa upande wa Alama za Biashara na Huduma ambazo hufahamika zaidi kama (logo) hizi mtu anaweza kukamilisha usajili wake kwa shilingi za Kitanzania 125,000.

Usajili wa alama hizi una faida lukuki katika soko la ushindani wa kibiashara kwa sababu unasaidia kuitangaza bidhaa husika na kuifanya ifahamike kwa wateja kama ni bidhaa na kama ni huduma kusaidia wale wanaohitaj waweze kuifikia kwa urahisi pale inapohitajika.

Naye Bi. Mariam Swalehe Said, Mkuu wa Idara ya Uhasibu katika chuo hicho aliipongeza BRELA kwa juhudi zake za kutoa elimu kwa umma na uhamasishaji wa urasimishaji wa biashara kwa sababu ni muhimu sana kwa vijana ambao wameanza masomo na wanaoelekea kumaliza masomo.

"Elimu hii itawafungulia njia mpya wanafunzi wa chuo, badala ya kusoma masomo ya darasani pakee sasa wanapata fursa ya kufahamu pia upande wa pili wa kuna vitu gani wanapaswa kufanya, nawashukuru sana BRELA kwa elimu hii," alisema Bi. Mariam.

Katika urasimishaji wa biashara BRELA imepewa majukumu kwa mujibu wa sheria kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Leseni za biashara kundi A, Leseni na Viwanda na Hataza.

Huduma zote hizi zinatolewa kwa njia ya mtandao ambapo mhitaji anatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa taifa (NIDA), anuani ya barua pepe, namba ya simu ya mkononi inayofanya kazi na baada ya hapo atatakiwa kutembelea tovuti ya BRELA yenye anuani www.brela.go.tz ili kuweza kufanya sajili.

**"Watu wengi wanafanya makosa wakati wa uanzishwaji wa biashara, mathalani kuanzisha na kutangaza biashara ambayo haijasajiliwa ni kinyume na taratibu kwa sababu kwa kufanya hivyo unaweza kuwa unavunja sheria kwa kutumia jina la mtu mwingine bila kujua au mtu mwingine anaweza kulisajili jina hilo na kulifanya lake kisheria"**



*Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kiisalamu Morogoro (MUM) wakisikiliza mada kutoka kwa Bw Yusuph Mwasakafyuka Afisa Usajili kutoka BRELA. Mafunzo hayo yalitolewa kwa lengo ya kuwaelimisha wanafunzi hao juu ya huduma zitolewazo na BRELA na namna ya kujisajili kwenye mfumo.*

# Watumishi wa BRELA waaswa kupima afya zao



*Watumishi wa BRELA wakisikiliza mafunzo ya namna ya kujali afya zao kutoka kwa mtaalam wa afya Dkt. Garvin Kweka kutoka Hospitali yaTaifa Muhimbili.*

**Na Sheila Mfunami**

Watumishi wa Wakala wa Usajili Biashara na Leseni (BRELA) wameaswa kuangalia afya zao kwenye mafunzo yaliyofanyika ukumbi wa mdogo wa Bunge jijini Dar es Salaam.

Mkufunzi kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Dkt Garvin Kweka aliwataka watumishi wa BRELA kujali afya zao na kuhakikisha mienendo yao ya kila siku haiathiri maisha yao kiujumla.

Aidha Dkt. Kweka alisisitiza kuwa kuna magonjwa mengi ambayo siyo ya kuambukiza lakini yamekuwa yakiathiri sana binadamu na kusababisha wengi wao kupoteza maisha na wengine kutofikia malengo pamoja na ndoto zao.

Licha ya kuwa wengi wakihofia kupata maambukiza ya ugonjwa wa ukimwi alisisitiza kuwa kuna magonjwa mengi makubwa zaidi ya UKIMWI yanayokatisha ndoto za wengi kama vile kisukari, moyo, figo, homa ya ini na mengine mengi yasiyoambukiza ambayo yamekuwa tishio kubwa sana na kukatisha ndoto za wengi.

Hivyo lengo kuu la kutoa elimu ya afya kwa watumishi wa BRELA ni kuwataka walinde afya zao pamoja kuangalia mienendo mizima ya maisha yao ya kila siku sababu wengi wamekuwa wakifanya kazi na kukosa muda wa kufanya mazoezi pamoja na kuzingatia milo kamili kwaajili ya afya zao.

"Kuna maradhi mengi yasiyoambukiza yanayopelekea wengi kuchukua hata maamuzi ya kujiua hii ni kutokana na msongo wa mawazo unaosababisha familia nyingi kuchukua hatua mkononi kwa aidha mama kunywesha sumu watoto kutokana na wivu wa mapenzi, wengine kuchoma visu wake zao na hata kujinyonga hii ni kutokana na watu wengi kushindwa kuhimili msongo wa mawazo inayopelekea wao kuchukua hatua moja kwa moja pasipo kujali matokea ya maamuzi," alisema Dkt. Kweka.

Akizungumza na washiriki wa elimu hiyo alieleza kuwa maisha ya sasa yamebadilika kutokana na utandawazi na siyo kama zamani. Sasa hivi mfumo wa maisha umebadilika na watu wanajali sana shughuli zao na kukosa muda wa kukaa karibu na familia zao, hasa malezi ya watoto ambapo imesababisha vijana wengi kuathirika kisaikolojia kutokana na mazingira wanayoishi. Sasa hivi kumekuwepo na ongezeko la wavuta bangi, mashoga, wanaojiuza pamoja na vibaka.

Aliwataka pia watumishi wa BRELA kupima afya zao mara kwa mara na kuzingatia mienendo ya maisha yao ya kila siku ili kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa.

Naye Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji Bw. Daimon Kisyombe Nathan Kisyombe alimshukuru Dkt. Kweka kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa kwa kuthamini afya za watumishi kwa kuwapatia elimu.

# Zingatieni sheria, taratibu na miongozo kuepusha kufanya makosa - Dkt. Michael




**Na Roida Andusamile**

Watumishi wa umma wametakiwa kufuata kanuni, taratibu, sheria pamoja na miongozo ya utumishi wa umma katika utendaji kazi wao wa kila siku ili kuepuka kutokufanya makosa ya kiutumishi.

Wito huo ulitolewa na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Francis Michael (pichani), ambaye kwa sasa ni Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii wakati akizungumza na wafanyakazi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) jijini Dar es Salaam.

Alitoa wito huo alipofanya ziara katika taasisi ya BRELA ikiwa ni sehemu ya utaratibu wa wizara yake ya kutembelea ofisi na taasisi za serikali ili kujua changamoto zinazowakabili watumishi wa umma katika sehemu zao za kazi.

Dkt. Michael alisema watumishi wa umma wanapaswa kufanya kazi kwa kufuata kanuni, sheria na taratibu ambazo zimewekwa kuepuka makosa ya kiutumishi.

Alisema kuwa Maafisa Utumishi wana wajibu wa kuwa na nyaraka zote za kiutumishi na kuhakikisha kuwa watumishi wote wanazifahamu nyaraka hizo kwa kuwa siyo nyaraka za siri.

Alisema hii itasaidia watumishi kujua haki, stahiki pamoja na wajibu wao na kuondoa uwezekano wa kufanya makosa ya kiutumishi kwa kutokutambua sheria na miongozo inayowasimamia.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itasaidia kuondoa malalamiko ya watumishi mahala pa kazi.

"Mtumishi anapokuwa na malalamiko ya kiutumishi ari ya kufanya kazi hupotea na hata malengo yaliyotakiwa kufikiwa na taasisi husika hayafikiwi kikamilifu. Ndiyo maana sisi viongozi kutoka utumishi tunaona ni bora tuwe tunawazungukia watumishi ili kuweza kuwafikia kwa ukaribu na kusikiliza shida zenu na kuyatatua mapungufu madogo madogo ambayo tunaona yanaweza kutekelezwa papo kwa papo," alisema Dkt Michael.

Pia, watumishi wa BRELA walitakiwa kuheshimu mamlaka kwa kufuata maadili na viongozi wanaowasimamia watumishi wa umma kutotakiwa kunyanyasa watumishi walioko chini yao kwa namna yoyote ile.

Aliongeza kuwa viongozi watambue kila mtumishi anatumia muda mwingi eneo la kazi na siyo nyumbani, hivyo kila kiongozi anawajibu wa kujenga mazingira mazuri sehemu zao za kazi ili watumishi waweze kufurahia kazi.

Alisema Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iko wazi kwa watumishi wote na itaendelea kutembelea taasisi za umma ili kusikia matatizo yao kwa lengo la kujenga na kuinua ari ya kazi kwa watumishi wa umma.

**"Mtumishi anapokuwa na malalamiko ya kiutumishi morali ya kufanya kazi hupotea na hata malengo yaliyotakiwa kufikia na taasisi husika hayafikiwi kikamilifu"**

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alifurahishwa kwa ujio wa Naibu Katibu Mkuu kwa sababu ni fursa nzuri ya kukutana na watumishi na kusikia changamoto zao kwa uwazi na kupatiwa ufumbuzi papo kwa papo.

# Mafanikio ya BRELA na Mwaka mmoja wa Rais Samia

- Yasajili kampuni 11,422 katika kipindi cha mwaka mmoja
- Urasimishaji wa biashara wafanyika kwa njia ya mtandao
- Yatoa usaidizi kwa Wawekezaji katika Kituo cha Pamoja kilichopo katika Kituo cha Uwekezaji (TIC)

Na Mwandishi Wetu

Mwisho wa safari moja ni mwanzo wa safari nyingine. Haya ni maneno ya wahenga ambayo tunayatumia kila siku, hasa tunapofurahia utimilifu wa jambo fulani na kuwa na mwanzo wa jambo lingine.

Katika kipindi cha Awamu ya Tano Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilitekeleza kwa kiasi kikubwa lengo la kuifikia dira ya Tanzania ya Uchumi wa Viwanda ambapo katika kipindi hicho idadi ya viwanda, kati ya mwaka 2015 na 2019 iliongezeka kwa asilimia 16 kutoka viwanda 52,633 mpaka 61,110.

Aidha, katika awamu hiyo pia BRELA ilitekeleza kwa kiasi kikubwa Mpango wa Serikali katika kuwarasimisha wafanyabiashara wadogo wadogo ili biashara zao zitambulike kisheria na kuwasaidia katika kupata fursa mbalimbali zinazopatikana kutokana na biashara kuwa rasmi.

Zoezi hili lilifanyika kwa kusajili Majina ya Biashara na Makampuni ya wafanyabiashara hao, pamoja na kuwapa elimu ya kufanya biashara zao kisasa kwa kufuata kisheria za nchi.

BRELA pia ilihamasisha wabunifu mbalimbali kuhusu kufanya usajili wa bunifu zao ili, pamoja na mambo mengine, ziwasaidie kukuza vipato vyao na pato la Taifa kwa ujumla.

Utimilifu wa safari ya Serikali Awamu ya Tano, ulianzisha safari ya Serikali ya Awamu ya Sita yenye dhima ya kukuza na kuimarisha zaidi biashara na uwekezaji nchini.

Unapotimia mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita, BRELA imeendelea kutengeneza na kuboresha mazingira rafiki kwa Wafanyabiashara na Wawekezaji hapa nchini na wa kutoka nje ya nchi.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa anasema kutokana na jitihada zinazofanywa na Rais wa Awamu ya Sita ya kuvutia biashara na uwekezaji nchini, BRELA pia imejipanga kimkakati kuhakikisha kuwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi wanaohitaji huduma zake wanahudumiwa kikamilifu ndani ya muda mfupi na gharama nafuu, kwa kutumia mifumo yake ya ki TEHAMA, ili waweze kuendelea na taratibu zingine za uwekezaji.

Bw. Nyaisa ameendelea kueleza kuwa kwenye Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC), BRELA pia ina dawati la huduma na imeweka Mtumishi anaetoa usaidizi wa haraka mara wawekezaji wanapofika kupata huduma katika Kituo hicho.

"BRELA tunathamini juhudi za Rais katika kukuza biashara na kuvutia wawekezaji, hivyo nasi tuko mstari wa mbele kuhakikisha kuwa mifumo yetu ya kiTEHAMA ya usajili na utoaji Leseni inafanya kazi kwa ufanisi ili kuongeza kasi ya urasimishaji biashara hapa nchini," alisema Bwana Nyaisa.



Yafuatayo ni mafanikio ya BRELA katika kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan:

## SAJILI ZA KIBIASHARA

BRELA imeendelea kuhamasisha usajili wa Kampuni nchini Tanzania ambapo kwa kipindi cha mwaka huu mmoja tangu Serikali ya Awamu ya Sita ishike hatamu ya uongozi jumla ya Kampuni ambazo zimesajiliwa ni 11,422 ikilinganishwa na idadi ya kampuni 9,478 zilizozajiliwa katika kipindi cha Machi 2020 hadi Februari 2021, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 21. Kati ya kampuni hizo, 11,348 ni Kampuni za Tanzania na Kampuni 74 ni za kigeni ambazo zimesajiliwa hapa nchini kwa malengo ya kufanya biashara na uwekezaji.

Utaratibu wa urasimishaji biashara umekuwa ni rahisi kutokana na mifumo ya kisasa ya kiTEHAMA ambayo inatumika kutoa huduma mbalimbali.

Wakati mwingine baadhi ya watu wamekuwa wakisita kusajili Kampuni kwa kuhisi kuwa mlolongo ni mrefu, lakini kupitia elimu inayotolewa kupitia mikutano, makongamano, maonesho na vyombo vya habari mbalimbali wamekuwa wakifahamishwa kuwa usajili wa Kampuni ni rahisi sana na hukamilika ndani ya siku tatu za kazi.

Mtu akiwa na fedha kiasi cha Shilingi 95,000 za Kitanzania, anaweza kusajili kampuni yenye mtaji usiozidi Shilingi 1,000,000 za Kitanzania. Vigezo vingine muhimu ni kuwa na namba ya utambulisho wa Taifa, hati ya mlipa kodi na katiba ya Kampuni.

BRELA imefanikiwa kuwafikia na kuwarasimisha wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali kupitia usajili wa Majina ya Biashara ili kuwafanya wawe rasmi katika kufanya biashara zao.

Katika eneo hili ndani ya kipindi cha mwaka mmoja imefanikiwa kusajili Majina ya Biashara 22,251

ikilinganishwa na Majina ya Biashara 20,364 yaliyo sajiliwa katika kipindi cha mwaka uliopita ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia tisa.

Jitihada hizi zinazofanywa na BRELA ni utekelezaji wa Ilani ya

Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) chini ya uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan inayosisitiza pia ufanyikaji wa mapinduzi ya kiuchumi kwa maendeleo ya watu.

Ibara ya 26(m) Sura ya Tatu inaelezea lengo la Serikali katika kurasimisha biashara za wananchi hasa wanyonge ili kuwawezesha kuondokana na umasikini kwa kutumia biashara zao kama dhamana katika taasisi za kifedha na kupata mikopo kwa ajili ya kujiendeleza.

Vile vile BRELA imeendelea kuwahamasisha watanzania kuhusu umuhimu wa usajili wa Alama za Biashara na Huduma pamoja na Hataza kwa ajili ya kulinda kazi zao za ubunifu na uvumbuzi na kupata haki ya kisheria ya umiliki wake.

Kutokana na jitihada mbalimbali za zinazofanywa na BRELA, kwa kipindi cha mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya sita, jumla ya Alama za Biashara 3,056 zimesajiliwa nchini Tanzania, ikilinganishwa na Alama za Biashara 2,033 zilizosajiliwa katika kipindi cha kuanzia Machi 2020 mpaka Februari 2021, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 50.

Uhamasishaji wa sajili hizi ni katika muendeleo wa utekelezaji wa Dira ya Serikali kama ilivyobainisha kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika ibara ya 48 (g).

Vilevile katika Ibara hiyo Serikali imeeleza wazi dhamira yake ya kurahisisha utaratibu wa utoaji Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara Kundi A kwa njia ya mtandao, jukumu ambalo linatekelezwa na BRELA.

Katika kutekeleza jukumu hilo, BRELA imeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu na faida za usajili wa viwanda vidogo na utoaji wa Leseni kwa ajili ya viwanda vikubwa kwa njia ya mtandao.

Kaguzi elimishi zimefanyika katika Mikoa ya Katavi, Rukwa, Pwani na Dar es Salaam na Wilaya zake, kwa kukutana na wamiliki wa Viwanda vidogo na vikubwa na kuwapa elimu juu ya urasimishaji wa viwanda vyao na pia kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Kwa upande wa Leseni za Biashara kundi A, zilitolewa 12,704 ikilinganishwa na Leseni 10,080 zilizotolewa katika kipindi cha Machi 2020 hadi Februari 2021 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 26. Hali hii ni dhahiri kuwa inatokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita za kuzidi kutengeneza mazingira rafiki ya biashara na kuhamasisha uwekezaji nchini.

## UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA WAMILIKI WANUFAIKA

BRELA imeendelea kusimamia zoezi la uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Wanufaika kwa kutumia mfumo wa kiTEHAMA. Zoezi hili linafanyika baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2020, kufanya marekebisho katika Sheria ya Makampuni na kuleta dhana ya Wamiliki wanufaika wa kampuni ambapo lengo kuu la dhana hiyo ni kuongeza uwazi katika taarifa za watu wanaonufaika na Makampuni ikiwa ni hatua mojawapo ya kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

## UBORESHWAJI WA MFUMO WA TEHAMA WA USAJILI

Ibara ya 48(g) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, imebainisha pia nia ya Serikali katika kurahisisha taratibu za usajili kwa kutumia mitandao ya TEHAMA.

Katika kutekeleza hilo, BRELA kwa kushirikiana na wataalam wa mifumo toka Taasisi mbalimbali za Serikali ilianza rasmi kubadilisha na kuboresha mfumo (System Re- designing) kwa nia ya kutatua changamoto zilizopo katika Mfumo unaotumika hivi sasa.

Kukamilika kwa maboresho ya Mfumo huo kutaweza kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto zilizojitokeza kwenye uliopo sasa.

Ili kupunguza usumbufu wa wahitaji huduma kuzunguka kwenye Taasisi kadhaa, Mfumo wa BRELA umeendelea kuunganishwa na mifumo ya Taasisi nyingine kama vile Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC),

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki mbalimbali, Uhamiaji na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazo husika na utoaji wa Leseni za Biashara za Kundi ‘B’.

## MUDA WA KUCHAKATA MAOMBI MBALIMBALI YA USAJILI NA LESENI

BRELA inatoa huduma sita ambazo ni usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Leseni za Biashara kundi A, Leseni za Viwanda, na Hataza.

Ukiachia zile ambazo Sheria zimeelekeza zikamilike ndani ya muda fulani mfano usajili wa Alama za Biashara na Huduma, huduma nyingine zote hukamilika ndani ya kuanzia siku moja mpaka 3 za kazi.

Ufanisi huo, kama ilivyo elezwa hapo awali, umetokana na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa Huduma hizo na mabadiliko ya mitizamo miongoni mwa Watumishi lengo kuu likiwa ni kuhakikisha kwamba Wafanyabiashara wengi zaidi wanapatahuduma za BRELA kwa sababu ndio miongoni mwa malango makuu ya kuanzia pale ambapo Wafanyabiashara, Wajasiriamali, Wawekezaji na wadau wengine wanapotaka kurasimisha biashara.

## KUHAMISHIA OFISI ZA BRELA KWENYE JENGO JIPYA

Katika kuhakikisha kwamba huduma bora zinatolewa kwa Wadau wake BRELA sasa imehamishia ofisi zake toka Jengo la Ushirika mtaa wa Lumumba kwenda kwenye jengo jipya lililopo katika makutano ya barabara ya Sokoine na mtaa wa Shaaban Robert jijini Dar es salaam.

Tangu BRELA ilipohamia katika ofisi hizo mpya mwishoni mwa mwezi Agosti, 2021 watumishi kwa sasa wanafanya kazi kwa nafasi na ufanisi na utoaji wa huduma umeongezeka.

Jitihada hizi zinazofanywa na BRELA ni sehemu tu ya utekelezaji wa mkakati mkubwa wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unaimarika kupitia biashara, ajira zinaongezeka, pato la taifa kupitia kodi linaongezeka, vilevile kasi ya uanzishwaji wa viwanda inaongezeka.

Ni dhahiri kuwa mafanikio haya yanayopatikana kwenye Taasisi yanachagizwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele sana katika kuhakikisha kuwa anavutia Wawekezaji na kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara hapa nchini.

**Wawekezaji, Wajasiriamali na Wafanyabiashara wote kutoka ndani na nje ya Tanzania, tembeleeni sasa tovuti ya BRELA yenye anwani mtandao ya www.brela. go.tz ili muweze kupata huduma hizi baada ya kutimiza masharti na mahitaji yote yaliyoainishwa kwenye kurasa za tovuti hiyo kama mkipata changamoto zozote msisite kuwasiliana na Kituo cha Huduma kwa Wateja kupitia namba ya simu ya mezani +255 (0) 222 212 800.**

# Mradi wa bomba la mafuta kunufaisha wananchi kupitia usajili BRELA



**Na Mwandishi Wetu**

Fursa mbalimbali za uwekezaji zinapojitokeza huwa na manufaa mbalimbali kwa wananchi walio jirani na maeneo husika kwani hufungua milango kwa wananchi kujipatia kipato kutokana na uwekezaji husika.

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga nchini Tanzania unaopita katika mikoa nane ya Tanzania Bara -- Kagera, Geita Shinyanga, Mwanza, Dodoma Singida, Tabora na Tanga -- ni mojawapo ya fursa ambayo Watanzania wanapaswa kuitumia kikamilifu katika kujiletea maendeleo binafsi na kwa taifa kwa ujumla.

Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, Aprili 11, 2021 walihudhuria hafla ya utiaji saini mkataba kati ya Serikali ya Uganda na Kampuni ya Mafuta Ghafi ya Afrika Mashariki juu ya utekelezaji wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la kutoka Hoima nchini Uganda kwenda Tanga nchini Tanzania. Mradi huo wenye urefu wa jumla ya kilometa 1,443 zikiwemo 1,115 zitakazojengwa ndani ya ardhi ya Tanzania, unatarajiwa kuzalisha ajira kati ya 6,000 na 10,000.

Fursa hii muhimu itawezesha Watanzania kupata ajira, kufanya biashara mbalimbali na kuongeza kipato. Hata hivyo fursa hizo zinapojitokeza wananchi wanapawa kufuata taratibu zilizopo ili kunufaika na bila kukumbana na kikwazo chochoto. Kwa upande wa wafanyabiashara kuna taratibu zinazopaswa kufuatwa hasa zile zinazosimamiwa na Serikali kupitia taasisi zake mbalimbali zenye lengo la kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ni miongoni mwa taasisi hizo, yenye jukumu la kuhakikisha kuwa inaweka mazingira mazuri ya biashara kwa mfanyabiashara kurasimisha biashara yake. Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Nyaisa anaeleza kuwa urasimishaji wa biashara unawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi na ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii.

Bw. Nyaisa anasema katika jitihada za kuweka mazingira rafiki kwa wadau wake BRELA imefanya maboresho makubwa sana katika mifumo yake na kiutendaji kwa kuwa imerahisisha taratibu za usajili kutoka analojia kwenda kidigitali kwani kwa sasa mfanyabiashara hapaswi kufika katika ofisi za BRELA ili kusajili badala yake usajili unafanyika kwa njia ya mtandao. “Urasimishaji wa biashara unawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi na ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii,” anafafanua Bw. Nyaisa.

Bw. Nyaisa anawasihi wafanyabiashara wadogo, wakati na wakubwa kutumia fursa ya mradi wa Bomba la Mafuta wenye manufaa kwa wafanyabiashara na kwa taifa kwa ujumla, kwani wanaporasimisha biashara zao mbali na kupata zabuni pia kuna fursa za mikopo katika mabenki kwani biashara zao zinakuwa zinaaminiwa, hivyo kuwa rahisi kukopesheka. BRELA inatumia fursa ya mradi wa Bomba la Mafuta kuwahamasisha wafanyabiashara

**"Urasimishaji wa biashara unawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi na ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii”**



kusajili majina ya biashara, majina ya kampuni na kupata leseni za biashara kundi A kwani katika miradi kama hiyo zabuni hutolewa kwa wafanyabiashara waliorasimisha biashara zao.

Aidha Afisa Mtendaji Mkuu anawakumbusha wafanyabiashara ambao tayari wamekwishasajili Makampuni au Majina ya Biashara kuwasilisha taarifa zao za kila mwaka (annual returns) kwa upande wa Makampuni na kulipia ada ya kila mwaka kwa wamiliki wa Majina ya Biashara (maintenance fees ) kama ambavyo inaelekezwa na Sheria zinazo simamia sajili hizo, vilevile amewataka wenye Makampuni ambayo yalisajiliwa nje ya mfumo (ORS) kuendelea na zoezi la kuhuisha taarifa za makampuni yao kwenye mfumo huo wa usajili kwani zoezi hilo ni muhimu kwenye kufanikisha utunzaji na upatikanaji wa taarifa sahihi za Makampuni.

Kwa upande wake Mkuu wa Idara ya Makampuni wa BRELA, Bw. Meinrad Rweyemamu anasema kuwa usajili wa jina la Biashara na jina la Kampuni hufanywa ndani ya siku tatu za kazi endapo nyaraka zote muhimu zinazohitajika zimewasilishwa kwa njia ya mtandao na kwa kuzingatia matakwa ya sheria na huduma husika.

Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao umepunguza gharama kwa wafanyabiashara ambao hapo awali iliwabidi kusafiri umbali mrefu kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kuja katika Ofisi kuu ya BRELA ili kukamilisha sajili na kupata leseni.

“Nyaraka zinazohitajika katika mfumo wa Usajili kwa njia ya mtandao (ORS) kwa upande wa jina la biashara Bw. Rweyemamu anazitaja kuwa ni kitambulisho cha Taifa, barua pepe, anuani alipo ya eneo la biashara na namba ya simu ya mmiliki na kwa upande wa kampuni ni kitambulisho cha Taifa, Hati ya kusafiria kwa wamiliki/ wakurugenzi wasio raia wa Tanzania, Utambulisho wa mlipa kodi (TIN) kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa wale watakao kuwa wakurugenzi wa kampuni, katiba ya kampuni (Memorandum and articles of Association) na Anuani za Wakurugenzi. Kuhusiana na gharama za usajili, Bw.Rweyemamu alieleza kuwa kwa sasa ada ya usajili wa jina la biashara ni Shilingi 20,000 na kwa upande wa usajili wa kampuni ada zimepangwa kulingana na kiwango cha mtaji uliotajwa kwenye katiba ya kampuni ( Memorandum) , mtu anaweza kusajili kampuni kwa ada ya chini ya kuanzia shilingi 95,000 endapo mtaji ni ule mdogo usiozidi shilingi milioni moja na ada ya juu kabisa ya usajili ni shilingi 440,000 endapo mtaji uliotajwa kwenye katiba ni zaidi ya shilingi milioni hamsini. Viwango hivi vya ada vimeorodheshwa kwenye tovuti ya BRELA yenye anuani www.brela.go.tz

Vilevile, Mradi wa Bomba la Mafuta utamwezesha mfanyabiasha kusafirisha bidhaa zake kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine na hata nje ya nchi hivyo kuwa na uhitaji wa leseni ya Biashara kundi A ambayo pia hutolewa na BRELA kwa njia ya mtandao kupitia Dirisha la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Portal-TNBP). Licha ya kutoa huduma zake kwa njia ya mtandao, BRELA mbali na ofisi za Dar es Salaam ambako ndiko Makao Makuu ya Taasisi, pia inatoa huduma ya usaidizi katika ofisi zake zilizopo kanda ya Kati, Ziwa na Kusini ambazo hutoa huduma kwa haraka kwa wafanyabiashara wanaopata changamoto katika mfumo. Katika kuhakikisha kwamba wadau wote wanapata usaidizi wa haraka katika kupata huduma, BRELA ina Kituo cha miito ya simu na huduma kwa wateja cha kisasa ambacho husaidia kutatua changamoto mbalimbali kupitia namba +255 (0) 222 212 800.

Sambamba na hilo BRELA imeweka utaratibu unaowawezesha wateja kuwasiliana kwa njia ya mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram, Twitter, WhatsApp na hata barua pepe) ambazo zinawawezesha wateja kuuliza swali na kujibiwa mara moja.

Mawasiliano kwa njia hizi zote hujibiwa ndani ya siku moja ili anayehitaji kukamilisha usajili wa aina yeyote aweze kukamilisha na kutuma maombi yake na kufanyiwa kazi kwa wakati.

# Jitihada za BRELA katika kukuza uchumi wa Tanzania

Biashara ni nguzo muhimu kwa taifa lolote duniani katika kukukuza uchumi wa nchi na kuleta maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Katika nchi ambayo biashara zimesimamiwa na kupewa kipaumbele zimekua zikisaidia kupunguza changamoto ya ajira kwa raia wake hivyo kusaidia kupata kipato cha kujikimu katika maisha yao.

Biashara pia ni chanzo cha mapato kwa serikali yeyote. Raia wengi wanapowekeza katika biashara serikali inapata mapato kupitia kodi na kuwekeza katika miradi ya maendeleo pamoja na huduma za kijamii.

Aidha biashara huboresha mahusiano ya nchi moja hadi nyingine kutokana na uuzaji wa bidhaa ndani na nje ya nchi, hii ni kwa sababu ya nchi moja au zaidi kutegemeana katika upatikanaji wa bidhaa za aina fulani.

Hizi ni baadhi ya faida kati ya nyingi za ustawi wa biashara katika nchi yeyote ambayo inatengeneza mazingira rafiki ya uwekezaji pamoja na ukuaji wa biashara zinazoanzishwa na raia wa nchi hizo au wageni.

Katika nchi ya Tanzania, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ni miongoni mwa lango la kuingilia kwa Wafanyabiashara na Wajasiriamali wakubwa na wadogo pamoja na wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa hivi karibuni amebainisha umuhimu wa kurasimisha Biashara, wakati alipofungua Kongamano la Wajasiriamali wanawake katika kuenzi siku ya Mwanamke Mjasiriamali Duniani.

Bw.Nyaisa amesisitiza kuwa urasimishaji wa biashara unawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi na ukuaji wa uchumi wa nchi na kuwa walipa kodi wazuri na washiriki wenza wa Serikali katika kutoa huduma kwa jamii.

“Serikali inaendelea kufanya maboresho bora ya Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu na mifumo ya utoaji huduma kwa kuzifanya kuwa wezeshi na rafiki kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo, ili waweze kurasimisha biashara zao na kunufaika na fursa mbalimbali zinazotokana na urasimishaji huo”.alifafanua Bw. Nyaisa.

Katika jitihada za kuweka mazingira rafiki kwa wadau wake BRELA imefanya maboresho makubwa sana katika mifumo yake na kiutendaji pia. Yafuatayo ni baadhi ya maboresho ambayo yamefanyika.

Mwaka 2018 BRELA iliachana rasmi na utaratibu wa utoaji wa huduma zake kwa njia ya makaratasi na kuanza kutumia Mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (Online registration system), pamoja na mfumo huu BRELA ilianzisha mfumo wa utoaji Leseni za biashara kundi ‘A” kwa njia ya mtandao kupitia Dirisha la Taifa la Biashara Tanzania National Business Portal (TNBP) mnamo tarehe 01 Novemba, 2019.

Mifumo hii ya usajili na leseni, ni sehemu ya uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Wafanyabiashara kote nchini sasa wanaweza kurasimisha biashara zao wakiwa popote.

Hii imepunguza gharama kwa wafanyabiashara ambao hapo awali iliwabidi kusafiri umbali mrefu kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kuja katika Ofisi kuu ya BRELA ili kukamilisha sajili na kupata leseni.

Katika kipindi ambacho mfumo huu wa ORS umeanza kutumika kumekuwa na mabadiliko chanya kwenye sajili na uthibiti wa ukusanyaji mapato kutokana na kutumia Mfumo wa Serikali wa kukusanyia mapato. Vile vile ongezeko hilo la sajili linaonekana kwani kwa mwaka 2018/2019 Wakala ilisajili kampuni 6,774 na Majina ya Biashara 11,591 ukilinganisha na mwaka 2020/2021, ambapo kampuni 9,754 zilisajiliwa na Majina ya Biashara 20,513.

Mafanikio hayo ni kiashiria tosha kwamba mfumo huu wa usajili kwa njia ya mtandao umekuwa chachu kubwa ya kuwavutia watu kufanya



*Afisa Mwandamizi kutoka BRELA Bi. Neema Kitala akitoa ufafanuzi juu ya usajili wa jina la biashara kwenye mfumo wa usajili wa BRELA kwa mmoja wa washiriki wa Mkutano wa Wanawake Wajasiriamali ulioandaliwa na Active Woman Foundation.*

sajili mbalimbali wakiwa katika maeneo yao ya kazi, nyumbani au mapumzikoni.

Hata hivyo; pamoja na mafanikio hayo, baada ya kuutumia mfumo kwa takribani miaka miwili, changamoto kadhaa zilibainika baada ya kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa Watumishi wa ndani, lakini pia wadau wa BRELA Mwezi Mei 2020, BRELA kwa kushirikiana na wataalam wa mifumo toka Taasisi mbalimbali za serikali ilianza rasmi kubadilisha na kuboresha mfumo (System Re-designing) kwa kuzingatia changamoto zilizopo katika mfumo unaotumika hivi sasa.

Kukamilika kwa Mfumo huo kutaweza kutatua changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na maombi kupokelewa na kufanyiwa kazi na Afisa mmoja, Ombi kufanyiwa kazi kwa kuzingatia ombi lililofika awali (first come, first served).

Kuendelea kuunganisha Mfumo wa BRELA na mifumo ya Taasisi nyingine kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), GePG, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki,TAKUKURU, Uhamiaji na Mamlaka za utoaji Leseni katika Halmashauri.

Lengo kuu ni kutengeneza mazingira rafiki na wezeshi sio tu kwa wawekezaji bali wafanyabiashara wote nchini. Licha ya kutoa huduma zake kwa njia ya mtandao, BRELA imefungua mlango mwingine kwa wafanyabiashara waliopo kanda ya kati ili kupata huduma kwa haraka na kuendeleza biashara zao.

BRELA imeandaa mkakati mzuri wa kuwahudumia wadau wa Kanda ya Kati, ikiwa ni pamoja na kuwatatulia changamoto wanazozipata wakati wa kufanya sajili mbalimbali katika mfumo wa ORS.

Ofisi ya Dodoma pia inahudumia mikoa ya jirani iliyopo Kanda ya Kati hasa katika kuwapatia elimu na kutoa usaidizi kwa wadau wake wote. Mbali ya Ufunguzi wa Ofisi ya Dodoma, BRELA pia ina ofisi katika mikoa ya Mwanza na Mtwara.

Katika kuhakikisha kwamba Wadau wote wanapata usaidizi wa haraka katika kupata huduma za BRELA, Kituo cha miito ya simu na huduma kwa wateja cha kisasa kilianzishwa ili kuwasaidia wote wanaokwama kwa namna moja au nyingine kuweza kutatuliwa changamoto zao.



*Afisa kutoka Wakala wa Usajili wa Bisahara na Leseni (BRELA), Bi. Sweetness Madata akiwasilisha Mada katika Mkutano wa wanawake wajasiriamali na Maonesho ya bidhaa yaliyoandaliwa na Active Woman Foundation.*

Kituo hiki kimewekewa mitambo ya kisasa ambayo humsadia mteja kupata usaidizi wa huduma yoyote kwa njia ya simu. Huduma hii imewekwa katika mfumo ambao umewezesha kuepusha msongamano wa simu nyingi katika njia moja.

Sambamba na hilo BRELA imeweka utaratibu mzuri kwa wateja ambapo wana uwezo wa kuwasiliana kwa njia mbalimbali zikiwemo njia ya mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram, Twitter, WhatsApp na hata barua pepe) ambazo zinamuwezesha mteja kuuliza swali na kujibiwa mara moja.

Mawasiliano kwa njia hizi zote hujibiwa ndani ya siku moja ili anayehitaji kukamilisha usajili wa aina yeyote aweze kukamilisha na kutuma maombi yake na kufanyiwa kazi kwa wakati.

BRELA inatoa huduma za Usajili wa Makampuni, Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Leseni za Biashara kundi 'A', Utoaji wa Leseni za Viwanda na Utoaji wa Hataza Huduma hizi zote hutolewa kwa kuzingatia matakwa ya sheria na huduma husika.

Mathalani, muda wa usajili wa Jina la Biashara ni siku moja (1) na si zaidi ya siku tatu (3) za kazi, Usajili wa Kampuni ni siku tatu (3) na si zaidi ya siku tano (5) za kazi.

Usajili wa Alama za Biashara na huduma ni kipindi cha siku 90 (kutokana na takwa la kisheria), maombi ya kupata Hataza ni siku 120 (kutokana na takwa la kisheria), kupata Leseni ya Kiwanda au Leseni ya Biashara kundi 'A 'ni siku moja (1) na si zaidi ya siku tatu (3) za kazi.

Taasisi inawajibu wa kuhakikisha kwamba Wafanyabiashara wengi zaidi wanapata huduma kwa sababu BRELA ndio lango kuu la Wafanyabiashara, Wajasiriamali, Wawekezaji na wadau wengine wengi.

Katika kuhakikisha kwamba huduma bora zinatolewa kwa Wadau wake BRELA imehamia katika ofisi mpya ambazo zinapatikana katika eneo la Posta Jijini Dar es Salaam, Kitalu Na 20, Nyumba Na 23, Makutano ya Mtaa

wa Shaaban Robert / Barabara ya Sokoine. Kuhamia katika Ofisi hii kumeongeza nafasi zaidi kwa Watumishi wa BRELA, uhifadhi wa Mifumo ya TEHAMA na hivyo kuongeza ufanisi zaidi katika utoaji wa huduma.

Pamoja na kuwa na Tovuti inayotumika sasa, Taasisi tayari inaendelea na ukamilishwaji wa Tovuti mpya ambayo itakuwa ni rahisi na itawasaidia Watanzania wote kupata taarifa wanazozihitaji katika tovuti hiyo.

Jitihada hizi zinazofanywa na BRELA ni sehemu tu ya mkakati mkubwa wa Taasisi wa kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unaimarika kupitia biashara ambako kutapelekea kuchangia ongezeko la ajira, vile vile pato la taifa linaongezeka kupitia kodi, pamoja na uanzishwaji wa Viwanda kukua kwa kasi.

Kama wahenga walivyosema "Kidole kimoja hakivunji chawa", na ndivyo itakavyokuwa hivi sasa ikiwa jitihada hizi zinazofanywa na BRELA wananchi hawatazipokea itakuwa ni sawa na kazi bure.

Watanzania wanapaswa kuchangamkia fursa zinazoambatana na urasimishaji wa biashara ikiwa ni pamoja na kupata haki za kipekee za umiliki wa biashara.

Fursa nyingine ni kwa wafanyabiashara kuwa na uwezo wa kutangaza biashara katika soko la ushindani, vilevile kupata haki

za kipekee za kulinda ubunifu au vumbuzi zao, kutambulika na Taasisi za kifedha mfano;' Benki wakati wa kufungua akaunti na kukopesheka. Pia urasimishaji biashara unaongeza wigo wa kufanya biashara kubwa mfano; biashara za kimataifa, kuongeza wigo wa kupata kazi na zabuni (tender serikalini na sekta binafsi) nakuaminika kwa wateja.

Vile vile urasimishaji biashara unamuwezesha mbunifu wa Alama kutambulisha na kutangaza bidhaa au huduma sokoni, Pia kuwawezesha watumiaji wa bidhaa kuitambua na kuichagua kwa kuangalia Alama moja na nyingine nyingi.




Tembelea sasa tovuti www.brela.go.tz ukiwa na namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), namba ya simu iliyo hai na anuani ya barua pepe iliyo hai ili kufungua akaunti yako na kupata huduma za BRELA na kama ukipata changamoto wasiliana nasi kupitia Kituo cha Huduma kwa Wateja kupitia +255 (0) 222 212 800

# Majibu ya maswali yaulizwayo mara kwa mara kuhusu wamiliki wanufaika

1. Nini maana ya Mmiliki Mnufaika?

Mmiliki Mnufaika (Beneficial owner) ni mtu ambaye anamiliki au kuhodhi moja kwa moja au kwa kupitia mtu mwingine zaidi ya asilimia 25% ya uwekezaji au ufanyaji maamuzi kwenye kampuni.

2. Je, hitaji la kutoa taarifaza Wamiliki Wanufaika linatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ipi?

Uwasilishwaji wa taarifa za Wamiliki Wanufaika unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Sura 212 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 pamoja na Kanuni za Wamiliki Wanufaika za mwaka 2021.

3. Nyaraka na fomu zipi zinapaswa kujazwa na kuwasilishwa wakati wa kuwasilisha taarifa za Wamilki Wanufaika?

Kampuni inapaswa kuwasilishataarifa za Wamiliki Wanufaika kwa kujaza fomu namba 14B inayopatikana kwenye tovuti ya BRELA. Aidha kampuni itapaswa kuwasilisha fomu namba 14C endapo Mmiliki Mnufaika huyo ameacha kuwa mnufaika kwenye kampuni au Fomu 14F endapo taarifa za mmiliki mnufaika zimebadilika.

4. Utaratibu upi unatumika kuwasilisha taarifa za Wamilki Wanufaika?

Taarifa za Wamiliki Wanufaika zinapaswa kuwasilishwa kwa njia ya mtandao kutumia mfumo wa Wamiliki Wanufaika unaopatikana kupitia https://bo.brela.go.tz au tembelea tovuti ya BRELA inayopatikana kupitia https://www.brela.go.tz.

5. Je, gharama zinazohitajika kuwasilisha taarifa za Wamilki Wanufaika ni zipi?

Gharama za uwasilishaji taarifa za Wamiliki Wanufaika ni Shilingi za Kitanzania 22,000/=

6. Je, kuna uthibitisho wowote unaotolewa na BRELA kuthibitisha kampuni husika imetekeleza hitaji la kuwasilisha taarifa za Wamilki Wanufaika?

Mwasilishaji atapokea risiti ya malipo ya uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Wanufaika kama uthibitisho.

7. Je, baada ya kuwasilisha taarifa hizo inachukua muda gani kupata majibu?

Wakala ikipokea taarifa inazichakata kwa lengo la kujiridhisha kama zimejazwa kwa usahihi kuziingiza kwenye daftari la siri.

Endapo kutakuwa na marekebisho kwenye kujaza taarifa hizo kampuni husika itapewa taarifa na kutakiwa kujaza kwa usahihi.

8. Je, kama kampuni haina Wamilki Wanufaika ifanye nini?

Ifahamike kwamba kila kampuni ina wamiliki Wanufaika, tofauti iliyopo ni aina ya Wamilki Wanufaika ambapo kampuni moja inaweza kuwa na wamilki wa moja kwa moja na nyingine ikawa na wamiliki wasio wa moja kwa moja.

9. Je, kampuni inapaswa kuwasilisha taarifa hizi kwa Msajili kila baada ya muda gani?

Taarifa za Wamiliki Wanufaika zinawasilishwa mara moja tu. Aidha kampuni itapaswa kuwasilisha taarifa kwa mara nyingine endapo Mmiliki Mnufaika ameacha kuwa mnufaika wa kampuni kwa kujaza fomu Na. 14C au pale Mmiliki Mnufaika ameacha kuwa mnufaika wa kampuni fomu kwa kujaza fomu Na. 14F.

10. Je, kuna madhara gani kama kampuni haiijawasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika?

Endapo kampuni itachelewa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika ifikapo tarehe 31 Disemba, 2021, itazozwa ada ya ucheleweshaji kiasi cha Shilingi za Kitanzania 2,500/= kwa mwezi kama ilivyoainishwa katika jedwali la ada kwenye Sheria ya Makampuni, Sura 212.

Hata hivyo, endapo kampuni itabainika na vyombo vya uchunguzi kuwa haikuwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika au iliwasilisha taarifa za Wamiliki Wanufaika zisizokuwa sahihi itakuwa imetenda kosa na baada ya kukutwa na hatia na Mahakama stahiki itatozwa faini kiasi kisichopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano na kisichozidi Milioni Kumi .

11. Je akaunti ya ORS inaweza kutumika kuwasilisha taarifa za Wamiliki wanufaika?

Mfumo wa uwasilishaji taarifa za Wamiliki wanufaika ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao. Hivyo mkurugenzi au katibu wa kampuni atapaswa kutengeneza akaunti mpya katika mfumo wa https://bo.brela.go.tz kisha kuingia na kuwasilisha taarifa hizo.

12. Je kama Mmiliki Mnufaika ni kampuni na sio mtu, utaratibu gani unatumika kuwasilisha taarifa hizo ?

Sheria inamtambua Mmiliki Mnufaika kuwa ni mtu mwenye halisi. Endapo kampuni au Taasisi ndiyo inayomiliki au kuhodhi umiliki kwenye kampuni, taarifa za wamiliki/watu wenye mamlaka ya ufanyaji maamuzi wa kampuni au taasisi hiyo watapaswa kutambulishwa kama Wamiliki Wanufaika.



*Afisa Mwandamizi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Raphael Mtalima akielezea umuhimu wa wafanyabiashara kuitumia taasisi ya BRELA katika kurasimisha biashara zao. Rai hiyo ameitoa kwenye mkutano maalum wa kusikiliza changamoto kati ya Taasisi wezeshi za biashara na wenye viwanda katika Maonesho ya Sita ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania-Zanzibar.*



*Afisa Mwandamizi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Raphael Mtalima akiwajengea uwezo wataalam wa kada ya uhasibu na ununuzi juu ya uzingatiaji wa sheria na taratibu za Makampuni zinazosimamiwa na BRELA, kwenye kikao kazi kilichoandaliwa na Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA) Dar es Salaam.*



*Maafisa wa BRELA wakijengewa uwezo wa namna ya kutumia mfumo wa e-mrejesho ambapo mfumo huu utatumika na wateja katika kutuma, kupokea na kufuatilia malalamiko, mapendekezo, maulizo na pongezi kwa huduma zinazotolewa na BRELA. Lengo la mfumo huo ni kuboresha huduma kwa mteja. Mafunzo haya yametolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA)*



*Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA ) wakipata mafunzo ya maadili, Kuzuia na kupambana na rushwa mahala pa kazi. Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo watumishi ili kufanya kazi kwa weledi na maadili kwa kufuata misingi ya sheria, taratibu na kanuni.*



*Watumishi kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wakiwa katika darasa la Mafunzo ya Huduma kwa wateja mahala pa kazi yaliyoendeshwa na kituo cha Mafunzo ya Utumishi wa Umma (Global Learning Centre kilicho chini ya Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) katika ukumbi mdogo uliopo katika Ofisi za TPSC jijini Dar es Salaam. Mafunzo haya yamelenga kuongeza ufanisi katika kutoa huduma bora kwa mteja.*

*Bw. Amos Bitea (kushoto) Afisa Uzalishaji kutoka Kiwanda cha Katavi Mining Company LTD akitoa maelekezo ya hatua za uzalishaji katika kiwanda hicho kwa Maofisa wa BRELA. Maofisa hao walifika katika kiwanda hicho kwa lengo la kutoa Elimu kuhusu urasimishaji wa viwanda. Katika sehemu ya elimu hiyo Bw. Bitea alielezwa kuwa Ili kupata Leseni ya Kiwanda au Cheti cha Usajili mwombaji anapaswa kulipia kulingana na kiwango cha Mtaji wa kiwanda husika*



**BRELA**

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI



Jengo la BRELA, Kitalu Na 20, Kiwanja Na 23
Mtaa wa Shaban Robert / Barabara ya Sokoine, S.L.P. 9393,
Ilala, Dar es Salaam. Simu: +255-22 2212800,
barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz ,

*Tovuti: www.brela.go.tz*